UTARATIBU WA KUPATA LESENI ZA BIASHARA

Leseni zote za Biashara hutolewa chini ya sheria ya Biashara Na. 25 ya mwaka 1972 na marekebisho yake yaliyofanyika Juni 2004 pamoja na marekebisho katika sheria ya fedha Na.2 ya Mwaka 2014 na Na.16 ya Mwaka 2015. Mwombaji wa leseni ya biashara anapaswa ajaze fomu ya maombi ya leseni TFN 211 (Business license application form).

Mtu yeyote raia wa Tanzania anayo haki ya kupatiwa leseni ya biashara ili mradi awe ametimiza umri wa miaka kumi na nane (18) mwenye akili timamu ambaye hajawahi kupatikana na kosa la jinai na awe na eneo la kufanyia biashara linalokubalika kisheria.

Kwa mtu ambaye sio raia wa Tanzania anapaswa kuwa na kibali kinachomruhusu kufanya biashara nchini kutoka IdarayaUhamiaji.

LESENI ZA BIASHARA ZIMEGAWANYIKA KATIKA MAKUNDI MAWILI:-

KUNDI A: Leseni hizi hutolewa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. (Fomu ya maombi iwasilishwe na kusainiwa na Halmashauri kabla ya kupelekwa Wizarani)

Mfano:

- Uagizaji bidhaa toka nje (import licence).
- Hotel za Kitalii (Tourist Hotel & Lodging).
- Wakala wa kupokea na Usafirishaji mizigo. (Clearing and Forwarding/ Freight Forwarders) n.k.

KUNDI B: Hizi hutolewa na Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji na majiji husika.

Mfano:

- Wakala wa Bima (Insurance Agent).
- Vipuri (Spare Parts, Machine tools).
- Maduka ya dawazaBinadamu/Mifugo Uuzaji Bidhaa Jumla na Rejareja (Wholesale and Retail trade) n.k.

UTARATIBU WA KUPATA LESENI ZA BIASHARA:

Kila mfanyabiashara anatakiwa afike katika Ofisi ya Biashara katika Halmashauri kwa ajili ya kuchukua fomu na kuzijaza kama utakavyoelekezwa. Baadhi ya nyaraka zinazohitajika kama kiambatanisho na masharti katika fomu ya maombi (TFN 211) ni:-

- Mfanyabiashara anapaswa awe na hati ya usajili iwapo anatumia jina la biashara (Certificate of Registration or Incorporation).
- Kama ni Kampuni mwombaji awe na *memorandum and: Articles of Association"* ambazo zinaonyesha kuwa kampuni imeruhusiwa kufanya biashara anayoiomba.
- Mwombaji awe na umri wa miaka 18 au zaidi.
- Awe na mahali/Eneoli na lokubalika kwa aina ya biashara anayoiomba na isiwe vibanda vilivyopo kando kando ya barabara.
- Awe na TIN *Certificate.*
- Awe na hati ya kuthibitisha uraia wake kama, Nakala ya Hati ya Kusafiria "passport" ya Tanzania, cheti cha kuzaliwa au Hati ya kiapo (Affidavit) au kitambulisho cha mpiga kura. Kama ni mgeni awe nahati ya kuishi nchini daraja la "A" (Resident Permit Class "A".)
- Masharti mengine ya kupata leseni hutegemea aina ya biashara mtu anayetaka kuanzisha, eg. Mgahawa, Dawa za Binadamu na Mifugo, Vyakula, Nyama na Samaki wabichi inabidi afuate taratibu zote za afya na kupima wafanyakazi wake.
- Hati ya utaalam (Professional Certificates) kwa biashara zote za kitaalam.
- Maombi mapya yatapitia ngazi za Serikali ya Mtaa, Mipango Miji, Afya na kasha Ofisi ya biashara kwa ajili ya utoaji wa leseni

- Cheti cha utakaso wa kodi "Tax Clearance Certificate" kutoka TRA

Kwa leseni zinazodhibitiwa na Mamlaka mbalimbali, Kwa mfano (TFDA, EWURA, TAURA, CRB, TILLI) n.k lazima mwombaji kuwa na leseni husika kabla ya kuomba fomu ya maombi ya leseni ya biashara (TFN 211).

Baada ya kujaza fomu na viambatanisho, maombi hupitishwa ngazi zinazotakiwa kisheria – Mpango Miji na Afya. Baada ya hapo leseni hutolewa kwa mfanyabiashara.

MALIPO: Kutokana na marekebisho ya sheria ya fedha Na 2 ya mwaka 2014 ada za leseni hulipwa kulingana na aina ya biashara.

MUDA WA LESENI: Uhai wa leseni ni miezi 12 toka siku ya kutolewa.

MASHARTI YA UTUMIAJI WA LESENI

1. Mwenye leseni hataweka masharti yeyote kwa mnunuzi.
2. Mwenye leseni atatoa risiti kwa mauzo yote.
3. Mwenye leseni atafuata sheria ya leseni ya Biashara No. 25 ya 1972.
4. Mwenye leseni hatatoa huduma/bidhaa ambazo hazizingatii viwango vya ubora, uliowekwa na vyombo vinavyotumika kisheria.
5. Mwenye leseni anaweza kunyang'anywa wakati wowote ikiwa itaonekana aliipatakwa njia ya udanganyifu au amekiuka msharti ya leseni.

MAKOSA

1. Kuendesha biashara bila leseni.
2. Kuendesha biashara eneo tofauti na linaloonyeshwa kwenye Leseni.
3. Kutumia leseni moja kufanyia biashara zaidi ya moja au maeneo mawili au zaidi.
4. Kushindwa kuonyesha leseni ya biashara inapotakiwa kufanya hivyo na Afisa aliyeidhinishwa na Serikali.

5. Kutokuweka leseni ya biashara mahali ambapo inaonekana kwa urahisi (KufichaLeseni).

6. Kumzuia Afisa wa Serikali aliyepewa mamlaka ya kukagua kufanya kazi yake.

ADHABU: Mtu yeyote anayetenda mojawapo ya makosa hapo juu adhabu yake ni faini isiyopungua Tshs. 50,000/= na isiyozidi Tshs. 100,000 au kifungo kisichozidi miaka miwili (2) au faini na kifungo kwa pamoja.

UMUHIMU WA KUWA NA LESENI KWA MFANYABIASHARA

1. Ndio kitambulisho kikuu cha mfanyabiashara ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
2. Ni moja ya nyaraka ya kisheria inayotumika na taasisi za kifedha ili kumpatia mfanyabiashara mkopo wa biashara.
3. Inaanisha aina ya Biashara na sehemu ambayo mfanyabiashara anafanyia kazi.
4. Kwa mfanyabiashara ili upate hati ya kusafiria ni lazima uwe na Leseni hai ya biashara.